MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA JUNI, 2018 NA MWELEKEO WA JULAI, 2018

Dondoo za Julai, 2018.

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Juni, 2018 na mwelekeo wa viashiria pamoja na hali ya joto kwa mwezi Julai, 2018 nchini.

a) Kwa mwezi Juni, hali ya baridi iliripotiwa katika maeneo mengi ya nchi kama ilivyotarajiwa katika utabiri, baridi kali zaidi iliripotiwa maeneo ya Nyanda za juu kusini magharibi ambapo kituo cha Igeri kilirekodi nyuzi joto 4 katika baadhi ya siku.
b) Hali ya joto la chini ya wastani inatarajiwa kwa kipindi cha mwezi Julai, 2018 hususan katika maeneo ya miinuko.
c) Vipindi vifupi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wote wa pwani ya nchi.

1. MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2018 NA MATAZAMIO YA MWEZI JULAI, 2018

1.1. MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2018

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2018 hali ya ubaridi iliripotiwa katika maeneo mengi ya nchi, hususan nyakati za usiku na mapema alfajiri, baridi kali zaidi iliripotiwa katika maeneo ya nyanda za juu kusini maghariribi. Mnamo tarehe 7 na 8 Juni, 2018 kituo cha Igeri (Njombe) kilipima kiwango cha nyuzi joto 4.3 na 4.2 vikiwa ni viwango vya chini zaidi vya joto kuripotiwa katika kipindi chote cha mwezi Juni, 2018. Mvua za nje ya msimu ziliripotiwa hususan katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini na yale ya ziwa Victoria.

2. MATAZAMIO KWA JULAI, 2018

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la chini ya wastani hadi wastani inatarajiwa kuendelea katika maeneo ya kati ya Kitropiki ya Bahari ya Pasifiki, ilihali hali ya joto la juu ya wastani inatarajiwa katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi, pwani ya Angola pamoja na pwani ya Somalia katika kipindi cha mwezi Julai, 2018. Hali hii ya joto la juu ya wastani katika bahari ya Hindi inatarajiwa kusababisha uwepo wa mvua za nje ya msimu katika ukanda wa pwani. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kuimarika na hivyo kusababisha vipindi vya upepo mkali pamoja na hali ya ubaridi katika maeneo mengi ya nchi.

2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2018

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2018 hali ya joto la wastani hadi chini ya wastani inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo vipindi vya baridi vinatarajiwa hususan nyakati za usiku na alfajiri.
Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 hadi 21 katika maeneo mengi. Hata hivyo baadhi ya maeneo ya miinuko ya mkoa wa Tanga hususan wilaya za Lushoto na Bumbuli zinatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 15. Hali ya ukavu kwa ujumla pamoja na vipindi kadhaa vya mvua za nje ya msimu inatarajiwa hususan katika wiki mbili za mwanzo za mwezi Julai, 2018.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 9 hadi 15 katika maeneo mengi. Hata hivyo baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango vya chini ya nyuzi joto 9. Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 18 katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango vya chini ya nyuzi joto 12. Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 18 katika maeneo mengi. Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa kuendelea.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 16 katika maeneo mengi. Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa kuendelea.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa na Mbeya): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 6 hadi 15 katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya miinuko pamoja na mkoa wa Njombe yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 6. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi, ingawa kuna uwezekano wa vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo ya miinuko (Tukuyu na Njombe).

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 hadi 21 katika maeneo mengi.
Hali ya ukavu kwa ujumla pamoja na vipindi kadhaa vya mvua za nje ya msimu inatarajiwa hususan katika wiki ya mwanzo ya mwezi Julai, 2018.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Viwango vya chini vya joto vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 9 hadi 15 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko ya mkoa wa Ruvuma yanatarajia kupata chini ya nyuzi joto 9 katika kipindi cha mwezi Julai, 2018. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea.

Imetolewa na;
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA